**OFISI YA RAIS TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE**
**<u>SHULE YA SEKONDARI USUKA - 2021</u>**

**S.L.P 226**
**NJOMBE**
**SIMU 0763853904**
**TAREHE ……………………..**

**KUMB.Na…………………………………………..**

**JINA LA MWANAFUNZI…………………………………………………………………….**

**S.L.P……………………................**

**WILAYA/MKOA………………………………….**

## <u>YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI USUKA ILIYOPO WILAYA YA WANGING'OMBE MKOA WA NJOMBE MWAKA 2021.</u>

### 1.0 <u>UTANGULIZI</u>

**Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza katika shule hii mwaka 2021 Shule ya Sekondari USUKA ipo umbali wa km 65 magharibi mwa Mkoa wa Njombe , Wilaya ya Wanging'ombe Usafiri wa basi Kutoka Mjini Njombe ni Tsh. 4000/=, Kutoka Makambako ni Tsh. 3000/=, Kutoka Ilembula ni Tsh.2000/=, Igwachanya Tsh.1500/= na usafiri unapatikana kwa Njombe kuna Basi la Lunyamadzo, Kwa Makambako kuna Basi la Fwilla, Wapendwa(Tesha) na Hiace (Msako) ya Makambako, Kwa Ilembula kuna Lupyana na Tumsifu.**
**Muhula wa Kwanza Masomo yanaanza Tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 17/01/2021 Ndani ya Siku saba.**

### 2.0 <u>MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA</u>

#### 2.1 <u>SARE ZA SHULE</u>

***A. WAVULANA***

- **Mashati meupe mawili (02) ya Mikono Mifupi**
- **Suruali Mbili rangi ya Dark Blue na Rangi ya Khaki (kama sare ya polisi) zenye Tun up(Upindo chini) sio Modo.Kitambaa namba moja vinginevyo wawaone mafundi wanaoelewa kitambaa Usuka.**
- **Sweta Rangi ya Kijani Jeshi na Begi au mfuko wa kubebea daftari sio kisalfeti**
- **Kiatu cheusi cha Ngozi chenye kisigino kifupi cha kufunga na kamba (sio raba)**
- **Soksi Nyeusi ndefu & Mkanda mweusi wa ngozi sio kitambaa.**
- **Daftari(Counter book) 4 au 5 na daftari za kawaida saba, Kalamu na Mkebe wa Hesabu**
- **Track Suit Nyeusi mterezo yenye michirizi miwili myeupe mabegani**
- **Aje na Ream bunda moja (A4) kwaajili ya mitihani ya mwezi, wiki na majaribio mbali mbali.(Ream zitakaguliwa na kukusanywa ni lazima)**

**Vifaa vya Michezo : Bukta na T.shirt yenye rangi yoyote ya Timu ya Taifa (T.F.F) na track suti nyeusi mterezo yenye michirizi myeupe. Track Suit ni Lazima kwa wote awe Hosteli au Day.**

***B: WASICHANA***

- **Mashati meupe mawili ya mikono mifupi**
- **Sketi mbili rangi ya Kijani Jeshi na Dark Blue (LINDA BOKSI IWE NDEFU INAYOFUNIKA SOKSI)**
- **Sweta rangi ya Kijani Jeshi Begi au mfuko wa kubebea daftari sio Kisalfeti**
- **Kiatu cheusi cha ngozi chenye kisigino kifupi cha kufunga na kamba sio Raba.**
- **Soksi Nyeupe ndefu**
- **Daftari(Counter book) 4 au 5 na daftari za kawaida saba, Kalamu na Mkebe wa Hesabu**
- **Aje na Ream bunda moja (A4) kwaajili ya mitihani ya mwezi, wiki na majaribio mbali mbali (Ream Zitakaguliwa na Kukusanywa ni Lazima).**
- **Vifaa vya michezo : Tshirt rangi yoyote ya Bendera au Timu ya Taifa / T.F.F na Track suti nyeusi mterezo yenye michirizi myeusi.(Track suit ni lazima kwa wote awe Day au Hosteli)**

**<u>ZINGATIA</u> : TRACK SUIT NI LAZIMA KWA WOTE NA ZITAVALIWA SIKU ZA MICHEZO .**

## ***2.2 <u>VIFAA VYA USAFI NA BUSTANI</u>***

- **Wasichana na Wavulana kila mmoja anatakiwa kuleta Kwanja moja jipya na kindoo kidogo (Lita kumi).Hakikisha unamkabidhi vitu hivi ajapo siku ya kuripoti shuleni kwaajili ya Usafi.**

## **2.3 *<u>CHAKULA</u>***

- **Kila mwanafunzi anatakiwa kuleta mchango wa Mahindi, Maharage na Fedha kama jedwali lioneshavyo ,**

| MAZAO | MUHULA WA 1 | MUHULA WA 2 | JUMLA(KWA MWAKA) |
|---|---|---|---|
| Mahindi | Debe 03 | Debe 02 | Debe 05 |
| Maharage | Lita 10(Nusu debe) | Debe 01 | Debe 1.5 |
| Fedha | 40,000/= | 30,000/= | 70,000/= |

- **Kama unaweza kutoa yote kwa mara moja au kwa nusu muhula ni uamuzi wako mzazi.**
- **Kwa mwanafunzi ambaye hatumii maharage tafadhali tuletee uthibitisho wa Daktari ili aweze kuangaliwa kwa upekee zaidi.**
- **Kila Mwanafunzi aje na SAHANI, KIKOMBE NA KIJIKO kwaajili ya chakula.**

**NB: Mzazi hakikisha mwanao ana Bima kwaajili ya Matibabu kama hana ,hakikisha unamuunganisha na wenzake ambapo watachangiana shilingi 2000/= kwa kila mmoja.**

**Pia hakikisha unampa nauli mwanafunzi kwaajili ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo kwa wanaosafiri zaidi ya umbali wa vijiji nje ya shule (kutoka nje ya kata au wilaya).**

## **2.3 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII**

**Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria namba .10 ya mwaka 1995 Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya WaziriMkuu-TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.**

**a) Heshima kwa viongozi, Wazazi ,Wafanyakazi wote,Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.**
**b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.**
**c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)**
**d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa**
**e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.**
**f) Kutunza usafi wa Mwili, Mavazi na Mazingira ya shule.**
**g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa**
**h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote**
**i) Kutunza mali za umma.**
**j) Ni marufuku kuleta vyakula vilivyopikwa shuleni na kuuza matunda yasiyotambulika na Utawala.**

**2.4 MAKOSA YAPELEKEAYO KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE**

**Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamisha shule.**

**a) Wizi**
**b) Uasherati na Ushoga**
**c) Ubakaji**
**d) Ulevi na matumizi ya madawa ya Kulevya kama vile uvutaji Bangi, Cocaine,Mirungi,Kubeli nk**
**e) Kupigana au Kupiga**
**f) Kuharibu kwa makusudi Mali ya Umma**
**g) Kudharau Bendera ya Taifa**
**h) Kuwa Mjamzito au Kupata Mimba**
**i) Kutoa Mimba**
**j) Kugoma, Kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na Usalama wa shule au watu**
**k) Kukataa Adhabu kwa makusudi**
**l) Kuwa na simu ya mkononi.**

**2.5 MAMBO MENGINE MUHIMU**

**Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi,**

**a) 'Medical Examination Form' ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.**
**b) Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu historia ya Mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika Migomo, Fujo na Makosa ya Jinai.**
**c) Fomu ya Mzazi kukiri kukubaliana na Sheria ,Kanuni na Maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.**

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**NB: Mzazi kama hujui vizuri kitambaa cha Unifomu za mwanao ni bora ukaja kushonea huku huku karibu na Mazingira ya shule kwani kuna mafundi wengi ambao wanajua kitambaa kinachotakiwa tafadhali hakikisha unanunua kitambaa namba moja orijino.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**…………………………………………**

**AMANI S. MWAKOMO**

**(MKUU WA SHULE).**

## FOMU NA.1 KUKUBALI AU KUKATAA NAFASI

**A. MWANAFUNZI**

1. **JINA KAMILI…………………………………………………………………………………………………………**
2. **Shule ya Msingi uliyosoma………………………………………………………………………………….**
3. **Namba ya Mtihani…………………………………………………………………………………………**
4. **Tarehe ya Kuzaliwa……………………………………………………………………………………..**
5. **Nakubali nafasi niliyopewa / Sitaki apewe tu mwingine (kata lisilohusika)**
6. **Nakiri / Naahidi kutoshiriki migomo, fujo na makosa ya jinai**
7. **Saini……………………………………………………………………………………………………………**

**B. AFISA MTENDAJI**

**JINA……………………………………………………………………………………………………………..**

**KIJIJI/KATA………………………………………….WILAYA…………………………..MKOA……………………….**

**Nathibitisha kuwa Mwanafunzi ……………………………………………………..……………..ni mkazi wa kijiji/mtaa/kata hii na ni raia wa Tanzania.**

**Sahihi…………………………………..Muhuri……………………………Tarehe…………………………………….**

**C. MZAZI/ MLEZI**

**JINA…………………………………………………………………………………………………………………..**

**Nakubali mwanafunzi apate elimu yake hapo Usuka Sekondari na kwamba atafuata Sheria, Kulipa michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule na vinginevyo aadhibiwe. Pia atalelewa katika dini ya …………………………………………………….**

## FOMU NA.2. TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

**JINA LA MWANAFUNZI……………………………………………………………………………………………………**

**TAREHE YA KUZALIWA……………………………………………………………………………………………………….**

**JINSIA…………………………………………………………………………………………………………………………**

**UMRI……………………………………………………………………………………………………………………………….**

**MAHALI UNAPOISHI……………………………..WILAYA…………………………………..MKOA………………………….**

**SIMU NA………………………………………………………………………………………………………………………………**

**JINA LA BABA……………………………………………………………….YUPO HAI?...........................................**

**JINA LA MAMA………………………………………………………………YUPO HAI?.........................................**

**ANUANI…………………………………………………SIMU NA……………………………………………………………………..**

**KAZI YA MZAZI / MLEZI…………………………………………………………………………………………………….**

**NB: TAARIFA ZA UONGO / ZISIZO SAHIHI ZITAPELEKEA MANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

## FOMU NA. 3 MEDICAL EXAMINATIONS

**(To be completed by medical officer only)**

1. **Pupil's Name…………………………………………………………………………………………………**
2. **Age………………………………………………………………………………………………………….**
3. **Blood Count(White& Red)……………………………………………………………………………….**
4. **Stool Examination…………………………………………………………………………………………**
5. **Syphilis or/ and other Veneral Diseases test……………………………………………………..**
6. **T.B test…………………………………………………………………………………………………….**
7. **Eye test…………………………………………………………………………………………………….**
8. **Ears………………………………………………………………………………………………………..**
9. **Abdomen………………………………………………………………………………………………….**
10. **Spleen…………………………………………………………………………………………………….**
11. **Urine for Plamo test……………………………………………………………………………………**

**ADDITIONAL INFORMATION**

**If any e.g Physical Defeats, Impairment, Infections, Pregnancy, Chronic or Family Diseases etc**

**……………………………………………………………………………………………………………………**
**……………………………………………………………………………………………………………………**
**……………………………………………………………………………………………………………………**
**……………………………………………………………………………………………………………………**

**I CERTIFY THAT THE ABOVE IS FIT TO PURSUE FURTHER STUDIES IN EDUCATION**

**STATION…………………………………………………SIGNATURE……………………………………………………..**

**DATE……………………………………………………DESIGNATION…………………………………………………..**